



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



**TAARIFA KWA UMMA**

**WANAFUNZI 7207 KUFANYA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE 2023**

Jumla ya watahiniwa **7207** wa Kidato cha nne katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, wameungana na wenzao nchini kote kufanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne mwaka 2023 ambao unafanyika kuanzia **Jumatatu, Tarehe 13 Novemba 2023** na utamalizika **Alhamisi, Tarehe 30 Novemba 2023**.

Kati ya watahiniwa hao 7207, **wavulana ni 3471, na wasichana ni 3736**, ambapo watahiniwa wa Shule ni **6869 (Wavulana 3332 na wasichana 3537)**, Watahiniwa wa kujitegemea ni **89 (Wavulana 25 na wasichana 64)**, na Watahiniwa wa mtihani wa maarifa (QT) ni **249 (Wavulana 112 na wasichana 137)** na vituo vyta kufanya mitihani vikiwa **63**.

Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela unawatachia kila la kheri watahiniwa wote wa Kidato cha nne 2023 katika mitihani yao ya kumaliza elimu ya Sekondari na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu wafanye vyema na huku wakizingatia taratibu zote za mitihani.

**Violencea S. Mbakile**  
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**  
**13 Novemba 2023**

---

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, 200 BR ya Buswelu, 33282 Buswelu,  
Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,  
Tovuti: [www.ilemelamc.go.tz](http://www.ilemelamc.go.tz)